³² Jironi parikitita juwa, wakuka nawo ka Insa piya wenye kuwa na mashetwani.

³³ Na piya wanu wa kaya ire wakijumana panryango.

³⁴ Basi, Insa akiwaponesa wanu wengi wa shida jisijisi, na akiwatuwisa mashetwani wengi. Iye aakiwasa mashetwani kusowera konta wakimwijija. §

Insa akwerezza Habari Ngema

³⁵ Subuu yake, Insa akilamuka alufajiri, akilawa nkaya mure, akúka mahala sapana wanu, akilebelu duwa nopo.

³⁶ Ansumani pamoja na wenziwe wakilawa kupita wakinsakula. Nakunsingana, wamwambira javi:

³⁷ "Wanu piya wankukusakula!"

³⁸ Fala Insa akiwajibu: "Tukeni mahala kwengine makaya mengine jirani ipate noko nikereze, konta noco omi ndi canijirire."

³⁹ Basi, akipita akerezza Habari Ngema mmasinagoga* mwawo na makaya piya a Galileya, na akiwatuwisa mashetwani.

Insa amponesa munu wa magundula

⁴⁰ Suku moja, kaja ka Insa munu mmoja camagundula, akinlebelu na akikokora mbere yake, akimwambira: "Ukisaka, kwanawo uwezo wa kuniponesa."

⁴¹ Neye akimmonera utungu, akolosa nkono wake akinkumbula, akimwambira: "Nisaka, swafika!"

⁴² Kwa mpunde noure, magundula are akimpakatika, munu ire akipona.

⁴³ Akinlaizira pakulu, akintuwisa,

⁴⁴ akimwambira: "Sikiriza! Usimwambire munu kinu. Ila ukarolote ka nlongozi wa dini, kapereke swadaka kamba vyayamba shariya ya Musa kwa kuswafika kwako uwé ushahidi kwavo."

⁴⁵ Fala nakulawa, camagundula ire akanza kutangaza, akeneza habari zire mpaka Insa aakidirire kwingira nkaya mure baina, fala kekala kunyenje mahala palanga. Wanu wakilawa kila upande wakimukira noko.

2

Insa amponesa munu wakuremala

¹ Paaludire tena Kafarnaumu, bandi ya suku aba, wanu wakipata habari kuwa kawapo nnyumba mwake.

² Wanu wengi wakijumana tapa-tapa, anta panryango aíkiwepo nafasi. Noparepare, Insa akikola kuwerezza usemi wa Mwenyezimungu.

³ Ikisa waja wanu wane wansukula kitewe mmashila.

§ ^{1:34} Ewo wakubali mamulaka ake. * ^{1:39} Sinagoga ndi nyumba ya duwa ya Mayahudi.

⁴ Kwa kuwa awakikidiri kufikisa paákiwa pare konta ya wanu, wakikwera papala wakitolola nopare paákiwa pare. Ikisa wakiteremusa mashila atandikiriwe kitewe ire.

⁵ Insa paawawonire wanu ware kuwa wantumaini iye, neye akimwambira nlwere ire javi: "Mwanangu, madambi ako aswamiiwa."

⁶ Na wákiwapo nopare wanlimu wa shariya wékala. Ewo wakiwaza mmyoyo mwawo, wakamba:

⁷ "Mbana asowera javi? Kakukufuru! Nani ari nawo mamulaka kuswamii madambi sairi Mwenyezimungu tu basi?"

⁸ Mpunde noure, pejije Insa cawari kuwaza mmyoyo mwawo, akiwambira: "Sababuni umwe kuwaza javyo mmyoyo mwenu?

⁹ Kumwambira kitewe-yu javi: 'Madambi ako aswamiiwa' au kumwambira: 'Lamuka, usukure mashila ako, uke vyako', sacirigariga ndi cepi?

¹⁰ Fala nukoloterani kuwa Binadamu wa Binguni kanawo mamulaka a kuswamii madambi mulumwengu-mu." Ndimana, kamwambira kitewe ire javi:

¹¹ "Uwe nukwambira: lamuka, usukure mashila ako, uke vyako ukaya."

¹² Neye akilamuka, kwa mpunde noure, akitwala mashila ake are, akilawa, wanu wakimmona javi. Wanu piya wakishanga, wakintkuza Mwenyezimungu, wakamba: "Tangu evi atinamba kuwona javi!"

Insa antapira Lawi amwita Matwaya

¹³ Sambi, Insa akilawa tena, akuka nanyenje ya tanda ra Galileya. Wanu wengi wawenye wakinfulata noko, neye akikola kuwafunda.

¹⁴ Paakuka nakupita, Insa kammona Lawi mwana wa Alufeu, ekare mahala pakiripisi-wanga nsoko. Iye akimwambira: "Nifulale!" Iye akilamuka akinfulata.

¹⁵ Ikisa, wakati mwengine, Insa pekare akirya nnyumba mwa Lawi-yu, wákiwapo wakirya naye pamoja na wanafunzi wake, warípisi nsoko wengi na wamádambi wengine.* Kusema kweli, awakifulatiwa na wanu wengi.

¹⁶ Sambi, wanlimu wa shariya wa kundi ra Mafarizeu, pawammonire kuwa kankurya na wamádambi pamoja na warípisi nsoko, wakiwadairi wanafunzi wake: "Sababuni kwikala na warípisi nsoko na wamádambi wengine kurya nawo?"

¹⁷ Insa, nakusikira, akiwajibu: "Wakomu awashugulika na dotoru, ila walwere. Onani, sijire kuwarifu wenye shariya wawe wanafunzi wangu, ila wamádambi."

Kukaidiyana kuhusu kufunga

¹⁸ Sambi, wanafunzi wa Yahaya mwenyé Koza na Mafarizeu wákiwa na tabiya ya kufunga. Suku moja, wanu wengine wakija ka Insa, wakindairi: "Wanafunzi wa Yahaya pamoja na Mafarizeu wafunga, fala wanafunzi wako-wa awafunga. Sababuni?"

¹⁹ Insa akiwajibu javi: "Warifiwe paharusi wari pamoja na mwenye-harusi, wafungaja? Mwenye-harusi akiwa pamoja nawo awajúzi kufunga.

²⁰ Fala ikuja kufika suku yakulaviwa mwenye-harusi-yo. Basi noyo suku-vo wakuja kufunga.

²¹ Aapo atáya kipande ca ngupo yagoma munguwo ya mida, kamana kipande kipyaco-cipapula ngupo ya mida, izidi kupapuka pakulu.

²² Aapo munu atwala maji a kazu saanasemuka kutairira nnumba zakumiya. Konta numba-zo zikipanjika, maji-vo atawanyika, na numba-zo zikwaribika. Kwa javyo maji-vo saanasemuka, tayani nnumba nyipya.†"

Insa suku ya sabadu

²³ Iwa suku moja, sabadu, Insa na wanafunzi wake wakipita nanyenje ya masamba a tirigu. Wanafunzi ware wakanza kuvunja masuke are watafune.

²⁴ Mafarizeu wakiwambira: "Ona, wanafunzi wako mbana watenda vinu savijuzi kutendiwa suku ya sabadu‡?"

²⁵ Fala Insa akiwajibu: "Amufyomire nkati ya Mandiko§ vyaatendire Daudi painkorire njala pamoja na weniwiwe?"

²⁶ Vyengire nNyumba ya Mwenyezimungu wakati Abiyatari wâwere nkulu wa wakulungwa dini. Katafuna mikate maalumu, yawákiwa nawo haki kutafuna walongozi wa dini tu basi. Ikisa mikate myengine akiwatongera weniwiwe."

²⁷ Ikisa Insa akiwambira: "Wanu awombiwe kwa ajili ya sabadu, ila suku ya sabadu itendiwa kwa ajili ya wanu.

* 2:15 Mayahudi wakikafilika naye konta mwenyé shariya aajuzi kurya na wamádambi. † 2:22 Ezi aya-zi, Insa kaamba nkinyume kuwa munu aifái kufulata tabiya zamida (kufulata shariya tu basi) iri kuwa iwapo namuna ya kuinshi mainsha mapya, julu ya kufulata njira yake. ‡ 2:24 Shariya ikataza wanu kukola kazi suku ya sabadu. § 2:25 Ona 1 Samuweli 21:1-6.

²⁸ Basi, Binadamu wa Binguni ndi Mwenye wa sababu.*"

3

Insa amponesa munu suku ya sabadu

¹ Sabadu nyengine, Insa akingira tena nsinagoga, nomure ákiwapo munu wakuremala nkono.

² Maaduwi wa Insa ware wakintunza sana-sana wammone kuwa amponesa suku ya sabadu ipate wanlaumu.

³ Noparepare iye akimwambira mwananlume wakuremala nkono ire javi: "Lamuka, uje kati-pa."

⁴ Ikisa piya ware akiwadairi javi: "Ihusu suku ya sabadu kutenda meema au mabaya? Kuvusha mainsha au kuulaya?" Fala ewo wakinyamala.

⁵ Insa akiwanang'aniza upande piya rungu-rungu akimiwe, akiuzunika kwa ajili ya myoyo yawo kuwa migumu. Ikisa akimwambira nlwere ire javi: "Olosa nkono-wo." Iye akolosa, akiponesiwa nkono wake ure.

⁶ Wakilawa Mafarizeu wakuka wakisowera na kinya Herodi. Wakijumana kuwazisana vyakumulaya Insa.

Wanu wengi viwajibu wammone Insa

⁷ Insa pamoja na wanafunzi wake wakilawa, wakuka kutanda ra Galileya. Wanu wengi wakinfulata, wanu wakulawa Galileya, Yudeya,

⁸ Yerusalem, Idumeya, ng'ambu nyengine ya Yordani, upande wa Tiru pamoja na Sidoni. Wanu wengi wasikire vinu vyakitenda, waja kummona.

⁹ Insa akiwambira wanafunzi wake wanvutire karibu yake ngalawa mmoja ipate wanu wasinkinye konta wákiwa wengi.

¹⁰ Kweli, wanu wengi wawenye káwaponesa, ndimana walwere piya wakimwirukira Insa wapate kunkumbula.

¹¹ Mashetwani, pawakimmona ponse, wakigwa mbere yake, wakikuwa wakamba: "Uwe kuwa Mwana wa Mwenyezimungu*!"

¹² Iye akiwashurutisa pakulu kuwa wasimwambire munu iye caari.

Insa awatondola mawali kumi na wawiri

¹³ Ikisa Insa akikwera mmwango, akiweta ware waawasakire iye mwanyewe. Newo wakija ka Insa.

¹⁴ Basi, iye akiwatondola wanu kumi na wawiri (ewo kaweta mawali) awe nawo, awatume wakerezee Habari Ngema,

¹⁵ na wawe nawo mamulaka akuwatuwisa mashetwani.

¹⁶ Wanu kumi na wawiri waâwatondore ndiwa: Ansumani (wantapire zina ra Peduru),

¹⁷ Yakobu mwana wa Zebedeyu, Yahaya nduye Yakobu wantapire zina ra Boanerge (mana ake "wana wa kuditima"),

¹⁸ Andere, Filipi, Bartolomeu, Matwaya, Tamimu, Yakobu (mwana wa Alufe), Tadeu, Ansumani nKanaa,

¹⁹ pamoja na Yuda Shikariyoti anzungunuke Insa.

Insa na Ibilisi

²⁰ Paaludire ukaya, wanu wengi wakijumana tena, awakipata anta nafasi ya kurya.

²¹ Jamaa zake pawasikire, wakilawa kuka kunkola, kamana wengine wakamba: "Ankili zimpoteya!"

²² Wanlimu wa shariya wa Yerusalem pawajire, wakamba: "Kanawo Belzebuli. Awatuwisa mashetwani julu ya uwezo wa nkulu wa mashetwani.‡"

²³ Sambi, Insa akiweta wanu, akikola kusowera nawo kwa vinyume, akiwadairi: "Shetwani antuwisa shetwani mwenzkiye mwaja?

²⁴ Kila ufalume wakwawayika makundi akubishana watupu, auinshi.

²⁵ Nyumba§ ikirawanya aiinshi.

²⁶ Ona, inawa Ibilisi aritendera vita mwanyewe kurawanya, singari kainshi, nanga uwa mwinsho wake.

* 2:28 "Mwenye wa sabadu" ári na mamulaka julu ya sabadu. * 3:11 "Mwana wa Mwenyezimungu" ndi zina rimojawapo retiwa Insa. Rikolota kupatana kwema ka Insa na Mwenyezimungu, kamba mwana na wawaye. Eri zina-ri aisema kuwa cipita kitendo ca muka na nlume, ila kupatana kukulu ka kiroho. † 3:22 "Belzebuli" Ibilisi au Shetwani.

‡ 3:22 Wakati-wo kuwatuwisa mashetwani ndi kinu cikikuna mara nyangi zawenye. § 3:25 "Nyumba" mana ake ujamaa.

²⁷ Aapo munu akidiri kwingira nnyumba ya munu wakurimba, kumwiwira vinu vyake sairi kwanza anfunga mwenyé nguvu-yo. Ikisa amwiwire sana nnyumba mwake.*

²⁸ Nukwambirani kuwa piya viswamiiwa ka wanadamu, madambi anta na kufuru zawakufuru wanu.

²⁹ Fala akufurira Roho Takatifu, aashubutu kuswamiiwa, fala akuwa na madambi a milele.”

³⁰ Insa kaamba javire kwa kuwa wakamba, “Kanawo mashetwani.”

Jamaa wakweli wa Insa

³¹ Kwa suku-yo, wakija mamaye na wanduze Insa wakimira panja, wakintuma munu kumwita.

³² Neye kekala na wanu wengi wawenye wânzunguriza, wakimwambira: “Ona! Mamayo, wanduzo, na walumbuzo wawa panja pare, wankukusakula.”

³³ Iye akiwajibu: “Mama ndi wepi? Na wanduzangu ndi wepi?”

³⁴ Basi, iye akizungunuka akiwanang'aniza wekare wanzungurize ware, akiwambira: “Wawoneni! Ewa-pa ndi mama na ndi wanduzangu.

³⁵ Kamana ire aténda vyaasaka Mwenyezimungu, noyo ndi nduyangu na nlumbwangu na mama.”

4

Insa afunda kwa kinyume

Kinyume kuhusu nyari*

¹ Mara nyengine tena, Insa akanza kufunda nanyenje ya tanda. Wanu wengi wawenye wajumana karibu yake. Kwa javyo, iye akingira mungalawa, akikala mbahari. Piya wanu wákiwa nanyenje karibu ya maji.

² Iye akiwafunda wanu vinu vingi kwa mifano ya kinyume. Nkati ya kuwfunda kwake, ákiwambira javi:

³ “Sikirizani! Mwananlume kalawa koka kuvyala masamba.

⁴ Paakimwaya mbeyu ire, nyengine igwirira munjira, zija nyuni zilokota.

⁵ Nyengine igwirira mmawe, mahala samuna nsanga mwingi. Mpunde noure ilawa senge, kwa kuwa auwerepo nsanga.

⁶ Pariwarire juwa senge ire ilungula. Kwa kuwa mizipe aiwere yamana, yumiliya.

⁷ Mbeyu nyengine igwirira kati ya miwa. Miwa ire ikula, ikinya mbeyu ire. Ntamana apiere.

⁸ Nyengine igwirira munsanga warutuba. Ikula, inuru na ípa visumo, muti mmoja talatinii, mwengine sitini na mwengine visumo miya.”

⁹ Mwinsho kaamba: “Ári na masikiro a kusikira, asikire!”

Anzima ya kinyume

¹⁰ Wanu wengi pawokire vyawo, wengine wakinzunguriza pamoja na wanafunzi kumi na wawiri ware, wakindairi kinani cinsowerese kinyume cire.

¹¹ Insa akiwajibu: “Umwe mwijiwisiwa siiri ya ufalume wa Mwenyezimungu. Fala ka wanu wengine wa panja, vinu piya wafundiwa kwa kinyume.

¹² Ndi kamba vyaasema Mandiko, kuwa javi:

‘Kunang'aniza wanang'aniza fala awawona
kusikira, wasikira fala awereriwa.

Wasije kongoka wakipata kuswamiiwa.’ ”

Insa afafanula kinyume kuhusu nyari

¹³ Insa kawambira, kaamba: “Amwereriwa na mana a eci kinyume-ci? Sambi vinyume piya, musaka kwereriwaja?

¹⁴ Nyvari ndi ire ereza Habari Ngema.

¹⁵ Nanyenje ya njira mana ake ndi wanu wasikira usemi uvyyariwe ure, nakusikira mpunde-sinkulu akuja Ibilisi awalavya habari yawavyariwe ire.

¹⁶ Na ewa ndi mbeyu ivyariwe mmawe, ndi wanu wasikira usemi, mpunde nowo wapokerera ka radi,

¹⁷ fala awana nzipe waho wanyewe, wainshi nawo suku aba. Ikija tafauti au kulumbat-iwa kwa sababu ya usemi wa Mwenyezimungu, mpunde nowo wabugudika.

¹⁸ Na wengine mbeyu ivyariwe mmiwa, ewa ndi wasikira usemi,

¹⁹ fala kwa tafauti za enzi-zi na wájibu wakupata mali na vinu vyengine, vikimwingira vikinya usemi ure, aupa visumo.

* 3:27 Insa aarikwamba kuwa vyema kwiwa nyumba. * 4: Au: “Nfano”.

²⁰ Na ware wavyariwe munsanga warutuba, mana ake ndi wasikira usemi wa Mwenyezimungu, wapokerera na wakupa visumo talatini, au sitini au miya.”

Kinyume kuhusu kandiyeru

²¹ Ikisa Insa akiwadairi: “Kandiyeru ikikoreziwa itaiwa nkati ya tamboru au ituriwa mwivivungu? Níkamba ikwangikiwa paarami imwarike sana.

²² Kusema kweli, acipo kinu cakufisiwa sacifisuriwa. Aipo siiri sailawira panja.

²³ Ári na masikiro a kusikira, asikire!”

²⁴ Akiwambira tena: “Tunzani camuri kusikira-ci. Kipimo camupimira nomwe mupimiriwa noco na mukongeziwa.

²⁵ Kamana ári nawo, azidi kupewa. Fala saana, anta aba caari nawo noco, anyang’anyiwa.”

Kinyume kuhusu mbeyu ya kukula

²⁶ Insa akamba tena: “Ufalume wa Mwenyezimungu ulandana na munu vyaaalya mbeyu pansi.

²⁷ Akilala usiku, nsana akilawa, kuno mbeyu ire ikiwota na ikikula, iye sejiwa.

²⁸ Ardhi iruwerya visumo wanyewe: cakwanza ulawa nnyani, ikisa suke, mwinsho wa suke ulawa mpunga.

²⁹ Mbeyu wakati waitokota, mpunde nowo munu akwanza kusinja kamana mavuno afika.”

Kinyume kuhusu mbeyu ya mostarda

³⁰ Insa akiwambira: “Kinani canisaka kulandanisa ufalume wa Mwenyezimungu? Ulandana na nfanoni?

³¹ Ulandana na mbeyu ya mostarda[†] paivyariwa pansi, ikuwa mbeyu noto javi. Ingawa mbeyu noto pakulu koliko mbeyu piya,

³² fala ikivyariwa pansi, ulawirira nrayi, úkula upunda mirayi piya. Ukuwa na vitambi vikulu, anta nviri wake nyuni zakwiruka julu zijenga vitundu nomo.”

³³ Na kwa kinyume cingi kamba noco, iye ákiwasowerera usowezi vyakujuzi ewo kupata kusikira.

³⁴ Bila usowezi wa kinyume aakisowera nawo. Fala paákiwa yeka ponse na wanafunzi wake, iye akiwereza mana awo kinyume caasowere cire.

Insa anyamaza mepo

³⁵ Noire suku ire jironi, Insa kawambira wanafunzi javi: “Tukeni tilokere ng’ambu nyengine ire.”

³⁶ Bandi ya kulayana na wanu wengi, ewo wakingira mungalawa mwákiwa mure, wakuka. Zikiwepo ngalawa nyengine nopo.

³⁷ Rikija gaibu rikulu, mawimbi makulu-makulu akikola kupanja ngalawa ire, anta maji akanza kwingira mungalawa mure.

³⁸ Na kumbe Insa ákilala pasitiri, kényamira nsawo. Wanafunzi ware wakinlamusa, wakimwambira: “Mwanlimú, tankufwa, mbana avikuyeri?”

³⁹ Noparepare akilamuka, akamuru mepo na maluwimbi, akamba: “Kutengemane, mepo inyamare!” Na mepo ire ikinyamala, kukitenda shuwari dembwe.

⁴⁰ Iye akiwadairi: “Mbanu muwa wofi pakulu? Amunamba kwamini?”

⁴¹ Ewo wakopa pakulu futi, wakambirana watupu: “Noyu mwananlume wakuwa anta mepo na maluwimbi vinsikiriza-yu, nani?”

5

Insa amponesa munu wakumilikiwa na mashetwani

¹ Insa na wanafunzi wake wakifika ng’ambu nyengine ya tanda, inti yawákikalanga waGerasi.

² Insa nakwisuka mungalawa mure, mpunde nowo kasimanana na mwananlume wakumilikiwa na jini, ákilawa kumakaburi.

³ Noyo mwananlume-yo ákkalanga kumakaburi, ákiwa na nguvu, anta na unyolo hapana akikidiri kunfunga.

⁴ Mara nyngi zawenye, wanu wakinfunga na alucema pamoja na unyolo, fala iye akitupula alucema na unyolo akisayasayanga. Aawerepo munu wanguvu wakunzaidi iye.

⁵ Daima usiku na nsana kumakaburi na kumyangano, akinyangulanga kuno akirisinja mwanyewe.

⁶ Kwa suku-yo, akimmona Insa kitambo, akintuwirira akisujudi.

[†] 4:31 Ona Matwaya 13:31-32.

⁷ Ikisa akikuwa pakulu akamba: "Insa, Mwana wa Mwenyezimungu Nkulu, usaka unitende kinani? Nukulebelwa, kwa zina ra Mwenyezimungu, usinopepese."

⁸ Konta kâmwambira javi: "Uwe jini, nlawe eyu munu-yu!"

⁹ Ikisa Insa akindairi jini ire: "Ukwitiwa mwaja?" Iye akijibu: "Nikwitiwa 'Junudi', konta tiwa wengi."

¹⁰ Iye akinlebelwa Insa pakulu kuwa asintuwise ire inti ire.

¹¹ Karibu nopare úkiwapo mwango na nkono wa nguluwe nyingi zawenye zikirya nopare.

¹² Mashetwani ware wakinlebelwa Insa: "Tipereke kunguluwe kure tikawengire."

¹³ Iye akiwetikizira, mashetwani ware wakinlawa mwananlume ire, wakuka wakingira nguluwe zire. Ikisa, piya zire zikitwa zikicubukira ntanda, kiyasi ca nguluwe alufu mbiri zigwirira ntanda.

¹⁴ Wasunga wakituwa wakuka ukaya wakereza habari zire. Nkaya mure na mma-masamba wakilawa wanu wakuka kuwona vinkunire vire.

¹⁵ Wakija ka Insa, wammona mwananlume âpatiwe na mashetwani ire kekala, avarire nguwo sana-sana, ári na ankili zake. Basi ewo ukiwapata wofi pakulu futi.

¹⁶ Wawonire vinkunire vire, wakikola kuwereza vinkunire mwananlume wa mashetwani ire na nguluwe zire.

¹⁷ Wakanza kunlebelwa Insa alawe nkaya mwawo mure.

¹⁸ Insa paakiripakira mungalawa, munu âpatiwe na mashetwani ire akinlebelwa woke onse.

¹⁹ Fala Insa ampere rihusa, akimwambira: "Uka kawári wanu wa kwenu, ukawereze mambo akuténdere Mwenye na vyakuwonere utungu!"

²⁰ Na kweli, iye akúka vyake, akanza kwereza kaya ya Dekapoli* mambo makulu atendériwe na Insa. Basi, wanu piya wakitajabu.

Insa awaponesa mwanamuka na mwana wa Yairu

²¹ Insa pengire tena mungalawa akuka upande mwengine wa tanda. Nakufika nanyenje ya tanda rire, junudi ya wanu wakijumana karibu yake.

²² Akija munu mmoja nkati ya wakulungwa wa sinagoga wakitiwa Yairu. Nakummona Insa, akisujudi,

²³ akintafadali pakulu, akamba: "Mwanangu kankufwa. Njo, unture makono ipate apone, ainshi!"

²⁴ Insa akilawa naye. Wanu wengi wawenye wakinfulata, wakinkinya kila upande.

²⁵ Ákiwapo mwanamuka nlwere mbobo muda wa myaka kumi na miwiri.

²⁶ Iye kata bika pakulu kuritibisa mmatabibu wengi wawenye. Kapoteza vyákiwa nawo piya kuwaripa mafundi, fala aapatire fuweni, ulwera ukinzidi.

²⁷ Nakuka, paasikire kuhusu Insa, akija nyuma ya wanu ware, akinkumbula anzu yake.

²⁸ Konta akamba kimoyomoyo javi: "Omi nikiwayi kukumbula lupindo ra anzu yake, nípona."

²⁹ Kwa mpunde noure, kububuka ka damu kure kukinyamala, neye akifahamu mmwiri mwake kuwa kaponesiwa ulwera ure.

³⁰ Insa, mpunde noure, kafahamu neye kuwa uwezo wakuponesa unlawa mmwiri mwake, akiwanang'aniza wanu nyuma, akamba: "Akumbure anzu yangu nani?"

³¹ Wanafunzi wake wakimwambira: "Kwankuwawona wanu-wa wakukinya! Udairija nani akukumbure?"

³² Iye akinang'aniza kuno na kuno ammone nani ankumbure.

³³ Kwa javyo, mwanamuka ire, akopa kuno akitetema, kejwa cinkunire. Akimukira Insa, akingwirira mbere yake, akimwambira piya ukweli.

³⁴ Basi, iye akimwambira: "Nunu, kwamini kwako kukuvusha. Uka kwa salama. Uwe nkomo, usiwe nlwera tena."

Insa anziripusa ka wafwi mwana wa Yairu

³⁵ Insa kuno akisowera, wakifika wanu kulawa kunyumba ya nkulungwa wa sinagoga, wakimwambira: "Mwanawo kafwa. Unshumbuwirani mwani limu-yu?"

³⁶ Fala Insa azimmwerire habari zire, akimwambira nkulungwa wa sinagoga ire: "Usisusuke, nitumaini omi tu basi."

³⁷ Fala iye aalavire rihusa kunfulata munu mwengine ila Peduru, Yakobu na Yahaya nduye Yakobu.

³⁸ Wakuka wakifika kunyumba ya nkulungwa wa sinagoga ire. Insa kawona geshi za wanu, wengine wankurira pakulu-pakulu, kuno wengine wakirondongola.

* ^{5:20} "Dekapoli" mana ake ndi "Makaya kumi". Ona 7:31.

³⁹ Iye nakwingira, akiwambira javi: "Sababuni kutenda geshi kuno mukirira? Mwari-yo aafwire, kankulala."

⁴⁰ Wanu ware wakinkejeli, fala iye akiwalavira panja piya ware. Ikisa, akintwala wawaye pamoja na mamaye mwari ire, na wanafunzi wake waalongozane nawo, wakgingira mwaákiwa mwari ire.

⁴¹ Akinkola nkono mwari ire, akimwambira: "Talita, kumi", mana ake "Mwari, nukwambira, lamuka!"

⁴² Kwa mpunde noure, mwari ire akilamuka, akanza kwenenda! Ku! Iye ákiwa na hirimu ya myaka kumi na miwiri. Basi, wanu ware wakitajabu pakulu futi.

⁴³ Insa akiwamuru akiwalaizira pakulu kuwa wasimwambire munu vikunire vire. Novyo akiwambira wampe mwari ire cakurya aryé.

6

Insa akatariwa Nazareti

¹ Sambi Insa akilawa inti ire, akiludira kwavo Nazareti. Wanafunzi wake ware wakinfulata.

² Paifikire sabadu, akanza kufunda nsinagoga. Wengi pawasikire, watajabu pakulu. Wakamba: "Vini-vi vyankulawirira ndepi? Ndi wijiwifuni wapewe-yu? Maajuza kamba-ya aténda na makono ake-ya kankupata ndepi?

³ Sinoyu-yu karipinteru, mwana wa Mariyamu, nduye Yakobu, Yose, Yuda pamoja na Ansumani? Walumbu atiri kwikala nawo nkaya nomu?" Ewo wakibugudika naye.

⁴ Basi Insa akiwambira: "Nabii ainshimiwa kila upande, ila ainshimiwa kwavo na awamwishi mu wajamaa zake na wenziwe."

⁵ Kwa javyo, iye aakidiri kutenda anta maajuza mamoja, sairi kuwatula makono walwere wamojawapo, kuwaponesa.

⁶ Iye akiwatajabu pakulu kwa sababu ya kutowa kumwamini.

Ikisa, akilawa akipita akifunda mmakaya.

Insa awapereka mawalii kwereza Habari Ngema

⁷ Sambi Insa akiweta wanafunzi kumi na wawiri ware, akanza kuwapereka wawiri-wawiri. Akiwapa mamulaka a kuwatuwisa mashetwani.

⁸ Akiwamuru wasirisukuze kinu munjira ila ngombo tu basi. Wasisukure cakurya, wala nrumba wala nzuruku,

⁹ wasirisukuze nguwo mbiri ila wawe na viratu mmaulu tu basi.

¹⁰ Akiwambira novyo: "Mukifika mahala, nyumba yamusaka kufikira noyo, ikalani nomo mpaka suku yamusaka kulawa nopo mahala-po.

¹¹ Ikiba awakupokerereni na awakusikirizeni, pakulawa pumunani matako enu*, iwe ushahidi kwavo."

¹² Ewo nakulawa pare, wakipita wakereza kuwa wanu wajuzi watubiye.

¹³ Mashetwani wengi wakiwatuwisa, na walwere wengi wakiwamiminira mafuta kuno wakiwaponesa.

Kuulaiwa ka Yahaya mwenyé Koza

¹⁴ Sambi, nfalume Herodi akisikira habari kuhusu Insa kwa kuwa zina rake rikisifiwa pakulu. Wengine wakamba: "Yahaya mwenyé Koza kaziribuka ka wafwi, ndimana kankukunisha mambo a maajuza."

¹⁵ Fala wengine wakamba: "Eyo Aliysi." Na wengine wakamba: "Eyo nabii mwengine, kamba minabii wamojawapo wa mida."

¹⁶ Fala Herodi paasikire akamba: "Wanintupure kiswa omi, Yahaya mwenyé Koza, kaziripusiwal!"

¹⁷ Kamana Herodi mwanyewe kâwatumá masurudadu wakankore Yahaya wanfunge na wantaye nkabaloshu kwa sababu ya Herodiza, muka wa Filipi nduye Herodi, kwa kuwa kânlomba.

¹⁸ Ndimana Yahaya kamwambira Herodi javi: "Auna haki ya kunlomba nlamuwo."

¹⁹ Kwa javyo, Herodiza akitimiyana na Yahaya, vikimwajibu amulaye. Fala aakidirire,

²⁰ konta Herodi akimopa Yahaya, akijiwa kuwa iye mwananlume mmoja wa shariya na takatifu, ndimana akinkengera. Wakati waansikire Yahaya, Herodi akifazaika, fala novyo-sivyo vikimwajibu kunsikira.

²¹ Kwa suku moja Herodiza akiija akipata nafasi ya kumulaya, suku Herodi yaakitenda mwaka. Kwa javyo, akitenda jambo, akiwarifu mawaziri wake, wakulungwa wa masurudadu, na wanu wakuinshimiwa wa Galileya.

* **6:11** Kigeregu: "pumunani vunu riri mmaulu mwenu".

²² Pengire kuvina mwana wa Herodiza, Herodi vimwajibu pakulu pamoja na wawarífire. Ndimana nfalume ire akimwambira mwari ire javi: "Nilebele causaka conse, omi nukupa."

²³ Ikisa akilapira tena, akamba: "Causaka kulebela conse, anta paiwa nusu ya ufalume wang'u-wu, nukupa!"

²⁴ Nakulawa iye akindairi mamaye: "Nilebele kinani?" Mamaye akamba: "Lebela kiswa ca Yahaya mwenyé Koza."

²⁵ Basi mwana ire aklidura upesi ka nfalume nokure, akilebela akamba: "Nisaka munipe nginga sambi nopapa, kiswa ca Yahaya mwenyé Koza."

²⁶ Nfalume ire akiakifilika pakulu futi, fala kwa kuwa kâlapira mbere ya wanu warifiwe ware, aankatarire.

²⁷ Basi, kwa mpunde noure, nfalume ire akintuma surudadu na akamuru cikaje kiswa ca Yahaya. Surudadu ire akuka kukalaboshu, akitupula kiswa ca Yahaya,

²⁸ akija naco nginga, akimpa mwari ire. Iye akipokerera, akimpa mamaye.

²⁹ Wanafunzi ya Yahaya ware, pawasikire vinkunire mwanlimu wawo, wakuka wakitwala maiti a Yahaya, wakizika.

Insa awapa cakurya wanu alufu ntanu

³⁰ Mawali'i ware wakijumana mbere ya Insa, wakimwambira piya vyawakitenda na vyawakifunda.

³¹ Iye akiwambira: "Njoni yeka yenu pakiriziu, mupumuzike aba." Kamana wanu wákija na wákiudi wákiwa wengi, ewo awákiwa nawo anta nafasi yakurya.

³² Wakisuka mungalawa mure, wakuka mahala kiriziu wakipumuzika.

³³ Fala wanu wengi wâwawona pawakilawa na wawéjiwa. Basi, ewo wakilawa luwansi mmakaya mure, wakiwatuirira noko, wakifika kâbula ewo sawanamba.

³⁴ Basi, Insa nakwisuka mungalawa mure, kawawona wanu wengi wajumana, akiwawonera utungu pakulu konta wákiwa kamba makondoo sawana nsunga. Akanza kuwafunda vinu vingi vyawenye.

³⁵ Paripepire juwa, wanafunzi ware wakuka ka Insa, wakimwambira javi: "Epa maha-la-pa pakilanga-langa, na juwa rypepa futi.

³⁶ Wambre wanu-wa woke vyawo mmakwawo au mmasamba ári karibu ipate wakauze cakurya."

³⁷ Fala Insa akiwajibu, akamba: "Wapeni umwe-po cakurya warye!" Ewo wakamba: "Basi, tuke tikauze mikate ya jarajara miyateni tije tiwape watafune?"

³⁸ Iye akiwadairi: "Umwe mwanawo mikate myengapi? Ukani mukanang'anize." Nakuwona wakija wakisema: "Mitanu, na inswi mbiri."

³⁹ Basi, Insa akiwamuru wanafunzi ware wawambire wanu ware wekare makundi-makundi mmnyanyi miwisi mure.

⁴⁰ Piya ware wakikala makundi-makundi a wanu miya au amusini.

⁴¹ Insa nakutwala mikate mitanu ire na inswi mbiri zire, akinang'aniza julu, akishukuru, akimeya mikate, akiwapa wanafunzi wake ware wawatongere wanu ware. Na inswi mbiri zire akiwatongera piya ware.

⁴² Piya warya na wekuta.

⁴³ Wakilokotera pamoja vipande vyakubaki vyä mikate na inswi, vikalala kumi na viwiri vyakwijala tapa-tapa.

⁴⁴ Na watafune mikate wákiwa wanawalume alufu ntanu!

Insa akwenenda julu ya maji

⁴⁵ Kwa mpunde noure Insa, akiwalazimisha wanafunzi wake wengire mungalawa, walongorere ng'ambu nyengine, Betisaida, mpaka iye ese kulayana nawo wanu ware.

⁴⁶ Pawesire kulayana, Insa akuka pamwango kulebela duwa.

⁴⁷ Paripepire juwa, ngalawa ilongorere ire íkiwa kati-kati ya tanda, na Insa ákiwa yeka yake kungulu.

⁴⁸ Kwa kuwawona kuwa wankutaya magasiya kwa tafauti kamana úkiwa mbisho, alufajiri galu ntanzi, iye akiwokira kuno akenenda julu ya maji. Akenenda kamba asaka kuwapunda,

⁴⁹ fala ewo pawammonire akenenda julu ya maji, wakidaniza kuwa nsoka, wakanza kufula uto.

⁵⁰ Kweli, piya wammona na wasusuka pakulu futi. Fala kwa mpunde noure, Insa akisowera nawo, akiwambira javi: "Rimbani myoyo! Ndi nomi, musope kinu!"

⁵¹ Iye akingira mungalawa mure, na mepo ire ikinyamala. Ewo wakitajabu pakulu futi!

⁵² Kusema kweli, wákiwa sawanamba kwereriwa kuhusu mikate ire, kamana myoyo yayo íkiwa migumu.

Insa awaponesa wanu Genezareti

⁵³ Pawalokire wakifika kungulu ya ng'ambu nyengine, inti ya Genezareti, wakitaya nanga.

⁵⁴ Nakwisuka mungalawa mure, mpunde noure wanu ware wammanyira.

⁵⁵ Wakinipa, wakituwa piya mmakaya mure. Walwere wakiwasukula mmashila, wakuka nawo mahala pawasikire kuwa ndi paari Insa.

⁵⁶ Mwakipita Insa monse, mmakaya asaka kuwa onse na nvitongojo, mmabazari wakiwatula walwere wawo, wakintafadali nanga anzu yake wankumbure. Na piya wakinkumbula, wákipona.

7

Ámuri za Mwenyezimungu bora pakulu

¹ Suku moja, Mafarizeu pamoja na wanlimu wa shariya wamojawapo wálawa Yerusalem, wakijumana ka Insa.

² Ewo wawawona wanafunzi wamojawapo wa Insa wakirya sawatawade.

³ (Kamana Mafarizeu, na Mayahudi piya, awarya sawatawade sana-sana, kwa kutumira tabiya ya wazee wawo.

⁴ Nakuludi kubazari, ikiwa awatawade sana-sana, awakirya. Ziwapo tabiya nydingi zawenye zawaúifulata: kosa kopo, miringi na vyombo vy a shaba.)

⁵ Basi, Mafarizeu pamoja na wanlimu wa shariya wandairi javi: "Wanafunzi wako awafulata tabiya za wazee, sababuni kurya sawatawade mmakono sana-sana?"

⁶ Iye akiwajibu: "Nabii Izaya kasowera tangu-mida kuhusu umwe manafiki kamba vyavyândikiwe javi:

'Ewa wanu-wa wanitokuza nkanywa* tu basi,
fala myoyo yaho iwa baidi nami.

⁷ Akufái kinu kunitokuza kwawo,
wafunda mafunzo na shuruti za wanadamu.'

⁸ Ikisa Insa akiwambira: "Wakwasa ámuri za Mwenyezimungu, ila wafulata shuruti za wanadamu."

⁹ Akiwambira tena: "Mwanawo tabiya yakukatala ámuri ya Mwenyezimungu ipate tabiya zenu zisise!"

¹⁰ Kamana Musa kâsema:

'Mwinshimu wawayo na mamayo', na
'Munu wakunsowerera caputu wawaye au mamaye,
ahukumiwe kifo.'

¹¹ Fala umwe mukwamba kuwa munu akimwambira wawaye au mamaye: 'Vinu vyaniki-juzi kukupani umwe ndi Kurbani',

¹² mwankukataza munu kuwasaidiya wawaye na mamaye.

¹³ Kwa javyo, mwankufuja usemi wa Mwenyezimungu kwa tabiya zenu zamufunda. Na mwankutenda vinu vingi kamba novyo."

Insa afunda kuhusu uswafi wa moyo

¹⁴ Mara nyengine Insa kaweta wanu wanfike karibu yake, akiwambira javi: "Piya-mwe, nisikirizeni omi, ereriwani.

¹⁵ Hapani kinu cakuwa panja ya mwanadamu cakuwa cikimwingira mmwiri cintaya haramu. Ila vinu vinlawwa ndi vintaya haramu."

¹⁶‡

¹⁷ Sambi, nakutanuka junudi ya wanu ire, Insa akingira nnyumba, na wanafunzi wake wakindairi: "Kinyume-ci mana ake kinani?"

¹⁸ Insa akiwajibu: "Umwe novyo amwereriwe? Amwijiwa kuwa vya panja vikimwingira munu avintaya haramu?

¹⁹ Kweli, avimwingira mmoyo, ila vimwingira ntumbokulu ikisa vilawira nsintina." Kwa javyo, Insa kolota kuwa piya vyakurya halali kurya.

²⁰ Insa akamba tena: "Vinlawwa munu, ndi vintaya haramu.

²¹ Konta, mmoyo mwa munu, alawa mawazo akunyata: ceje, vivi, ukisomi,

²² uzinzi, wájibu wakupata vinu piya, ubaya, ulongo, wájibu wa vitendo vya ucaputu, wiyana, kufuru, kuridái pamoja na urevi.

* 7:6 Kigeregu: "mivumbu". † 7:11 "Kurbani" mana ake "Nilapira kumpa Mwenyezimungu". Ona Matwaya 15:5.

Wakati wa Insa, ikiwapo tabiya yakuwa munu wakuriturira kinu mbere alavye nadiri ka Mwenyezimungu, munu-yo aajuzi kuwasaidiya wawaze. Kusema kweli, tabiya-yo ibishana na shariya ya Musa yakuwatuwuza wawaze. ‡ 7:16 Mandiko mengine a mida aana aya-yi. [Ári na masikiro onse, asikire!]

²³ Vitendo vyakunyata-vi, piya vília wa mmoyo, ndimana vintaya munu haramu."

Mwanamuka mmoja Saari-Yahudi amwamini Insa

²⁴ Nakulawa pare, akukirira makaya a Tiru na a Sidoni. Iye nakwingira nnyumba, kasaka asijiwikane, falakini aakidirire kurifisa.

²⁵ Mwanamuka mmoja, akíwa na mwanaewe kápatiwa na jini, akisikira kuwa Insa kaja. Nakunfika akinkokorera mmaulu mwake.

²⁶ Mwanamuka ire aáwere Yahudi, kwawo kúkiwa Sirufoinike. Akilebelu atuwisiwe jini mwanaewe ire.

²⁷ Iye akamba javi: "Wase kwanza wasimana wekute. Kamana sivyema kutwala mikate ya wasimana, kuwefyera wawumbwa[§]."

²⁸ Mwanamuka ire akijibu akamba: "Aye, Mwenye, fala wawumbwa wakuryanga songolo za pansi zakuwagwa wasimana pameza."

²⁹ Basi Insa akimwambira tena: "Kwa sababu ya usowezi wako, mwanaeo katuwisiwa jini-yo futi. Ludi, uka ukaya."

³⁰ Mwanamuka ire nakuludira ukaya, kansingana kisimana ire alarire pakinanda, jini ire anlawire.

Insa amponesa munu bubu saasikira

³¹ Insa akilawa tena makaya a Tiru akija Sidoni, kutanda ra Galileya, kati-kati ya makaya a Dekapoli*.

³² Noparepare wakinjisira mwananlume mmoja bubu, saasikira. Wakinlebelu anture nkono†.

³³ Insa akintanusa pawantu pare, akuka naye kiriziu, akintaya vyala mmasikiro, akin-taya mata ake julu ya lulimi,

³⁴ akimwinula uso julu binguni, akimpumuzikira, akimwambira na luga ya kiyara-maiku‡: "Efata", mana ake "Ziuka."

³⁵ Kwa mpunde noure, masikiro akinziuka na nzipa wa lulimi ukinkunjuka, akanza kusowera sana-sana.

³⁶ Ikisa akiwamuru wanu ware kuwa wasimwambire munu. Fala kila paákiwamuru kuwa wasiseme, ndi pawakizidi kwereza.

³⁷ Kwa javyo, wakitajabu pakulu, wakamba: "Vitendo vyake piya vyema! Sawasikira awasikirisa, na mabubu awasoweresa!"

8

Insa awapa cakurya wanu alufu nne

¹ Nozire suku zire, iwa tena wanu wengi awákiwa nawo cakurya, Insa akiweta wanafunzi wake, akiwambira javi:

² "Wanu-wa niwawonera utungu konta wawa nomi suku natu, awana kinu cakurya.

³ Nikilayana nawo wakiludira mmamakwawo wafungire, awaja kuzirika munjira? Wengine waja kulawa baidi."

⁴ Fala wanafunzi ware wakinjibu: "Palanga kamba-pa, munu akidirija cakurya cakuweikutisa ewa wanu-wa?"

⁵ Insa akiwadairi: "Mwanawo mikate myengapi?" Ewo wakinjibu: "Saba."

⁶ Basi akamba: "Wanu piya wekare pansi." Akitwala mikate saba ire, akinshukuru, akimeya, akiwpa wanafunzi ware, newo wakiwatongera wanu ware.

⁷ Wákiwa nawo novyo inswi aba. Noparepare Insa akintukuza Mwenyezimungu, akisema: "Nezo novyo watongereni piya-wo."

⁸ Na wanu ware wakiryia wakikuta, mwinsho wakilokotera vipande, vikilawirira vikalala saba vyakwijala vyawenye.

⁹ Wanu wákiwa kiyasi ca alufu nne. Ikisa, akihayana nawo.

¹⁰ Kwa mpunde noure, iye akingira mungalawa pamoja na wanafunzi wake ware, akuka upande wa Dalmanuta.

Mafarizeu wanlazimisha Insa alama ya maaжуза

¹¹ Wakilawa Mafarizeu, wakuka wakikaidiyana naye. Ewo wakisakula alama ya bingu, wakimyerera.

¹² Kwa javyo, Insa akipumuzika pakulu, akamba: "Sababuni eci kizazi-ci kisákula alama? Nukwambiraní kweli kuwa kizazi-ci acoloteriwa alama."

§ 7:27 Mayahudi wawatula wanu piya Sawari-Mayahudi kamba makafiri, na mbere yayo umbwa ndi alama ya ucafu.

* 7:31 "Dekapoli" mana ake "Makaya kumi". Ona 5:20.

† 7:32 Kuntula nkono ndi alama ya kunlebelela

Mwenyezimungu anjanliye na amponese.

‡ 7:34 "Kiyaramaiku" luga yakutumika Insa nowo wakati-wo.

¹³ Basi, akiwasa, akiripakira tena, akuka ng'ambu nyengine.

Furumento ya Mafarizeu na ya Herodi*

¹⁴ Na kumbe, wanafunzi ware wariwala kusukula cakurya. Mungalawa mure wákiwa nawo nkate mmoja tu basi.

¹⁵ Insa akiwalaizira, akamba: "More-moreni na furumento ya Mafarizeu pamoja na ya nfalume Herodi."

¹⁶ Wakikola kukaidiyana watupu konta awâwere nawo mikate.

¹⁷ Insa, pejiwe kuwa wankuaidiyana, akiwambira: "Mbanu mukaidiyana kwa kutowa kuwa nawo mikate? Amunamba kwijiwa mana wala amunereriwa? Myoyo yenu migumu pakulu?

¹⁸ Umwe mwanawo maso, amuwona? Mwanawo masikiro, amusikira? Amukumbukira?

¹⁹ Mikate mitanu yaniwatongere wanu alufu ntanu ire, vipande víbakire víjala vikalala vyengapi?" Ewo wakijibu: "Kumi na viwiri."

²⁰ "Na mikate saba kwa wanu alufu nne, vipande víbakire víjala vikalala vyengapi?" Ewo wakijibu: "Saba."

²¹ Basi iye akiwambira tena: "Mpaka sambi amunamba kwereriwa?"

Insa amponesa kipofu

²² Insa na wanafunzi wake wakifika Betisaida. Wakija nawo ka Insa munu mmoja sawona, wakinlebelia ankumbure.

²³ Iye nakunkola nkono sawona ire, akinlongoza nanyenje ya kaya ire. Nakunsunira mata mmaso, akintula makono, akindairi: "Kwankuwona kinu kimojawapo?"

²⁴ Mwananlume ire akinang'aniza julu, akamba: "Nankuwawona wanu kamba miti íri kwenenda!"

²⁵ Ikisa tena, akintula makono julu ya maso ake. Munu ire akinang'aniza rungu-rungu, akiponesiwa, akanza kuwona piya vinu sana-sana.

²⁶ Insa akimwambira: "Epa, uka nfululu kwenu, usipite nkaya tena."

Peduru atangaza kuwa Insa Almasihi

²⁷ Insa na wanafunzi wake wakuka mpaka makaya a Kaisariya-Filipi. Munjira iye akiwadairi, akamba: "Wanu wakwamba kuwa omi niwa nani?"

²⁸ Ewo wakinjibu: "Wengine wakwamba uwe kuwa Yahaya mwenyé Koza, wengine wakwamba kuwa Aliyasi, na wengine wakwamba kuwa nabii mwengine mmojawapo."

²⁹ Insa akiwadairi tena: "Sambi, umwe mudaniza kuwa omi niwa nani?" Peduru akinjibu, akamba: "Uwe ndi Almasihi!"

³⁰ Basi, Insa akiwalaizira kuwa wasimwambire munu kuhusu iye caari.

Insa asowera kuhusu kifo cake na kufufuka kwake

³¹ Sambi, Insa akanza kuwafunda kuwa Binadamu wa Binguni ajuzi atabike pakulu, akatariwe na wazee, wakulungwa wa dini, pamoja na wanlimu wa shariya. Ikisa ajuzi aulaiwe, fala bandi ya suku natu afufuke.

³² Iye akisowera evi vinu-vi bila kuwafisa. Fala Peduru akimwita kunyenje, akanza aulutumu.

³³ Insa akizungunuka, akiwanang'aniza wanafunzi ware, akinsutumu Peduru, akamba: "Lawa-pa uka nyuma-ko, Shetwani! Kamana auwaza mawazo a Mwenyezimungu ila a wanadamu!"

³⁴ Ikisa akiweta wanu ware pamoja na wanafunzi wake akiwambira javi: "Ikiwa munu mmojawapo asaka kunifulata, arikane mwanyewe, asukure nsalaba wake, na anifulata.

³⁵ Kamana asáka kuvusha mainsha ake, apoteza. Fala apotéza mainsha ake kwa sababu yangu omi na ya Habari Ngema, ávusha.

³⁶ Munu kupata duniya nzima-yi, kupoteza mainsha ake, faidani?

³⁷ Munu cakakanya na mainsha ake kinani?

³⁸ Munu akiriwónera haya nomi au usowezi wangu kati ya eci kizazi ca uzinzi na dambi-ci, Binadamu wa Binguni, pakuludi na utukufu wa Baba na malaika matakatifu, iye novyo akuja kuriwonera haya naye."

9

¹ Insa akiwambira, akamba: "Nukwambirani kweli kuwa wawapo nopapa wamjawapo aciwapata kifo viwa vyonse sawawonire ufalume wa Mwenyezimungu ukija na uwezo."

* ^{8:13} "Furumento" ndi alama ya dambi yakuwa na nguvu zakukula.

*Kutaduka ka Insa**

² Bandi ya suku sita, Insa akiwatwala Peduru, Yakobu, pamoja na Yahaya, akiwalongoza kumwango nrefu kiriziu, yeka yawo. Akitaduka mbere yawo,

³ mavazi ake akimensa, ákiwa melupa pakulu vú koliko kinu cisaka kuwa conse duniya-yi.

⁴ Nopare, wakilawirira nabii Aliyasi pamoja na Musa, wakanza kupakanira na Insa.

⁵ Sambi Peduru akamba: "Mwanlimu, vyema tikare nopa! Tijenge vibanda vitatu: kimoja cako, cengine ca Musa, na cengine ca Aliyasi."

⁶ Kusema kweli, Peduru aakijiwa caakisowera konta wanafunzi ware piya uwapata wofi pakulu.

⁷ Rikija wingu rikiwafinika. Nkati ya wingu ikisikirika shauti ikamba: "Eyu ndi Mwanangu wanimpenda. Nsikirizeni!"

⁸ Kwa mpunde noure, wanafunzi ware wakimangamanga kunang'aniza, wammona Insa tu basi ari pamoja newo.

⁹ Pawakisuka pamwango pare, Insa kawambira kuwa wasimwambire munu vyawawonire vire, Binadamu wa Binguni saanamba kufufuka ka wafwi.

¹⁰ Ure usowezi ure wakitula ila wakikola kukaidiyana watupu mana a usowezi wa "kufufuka ka wafwi".

¹¹ Ikisa wakuka wakindairi Insa: "Sababuni wanlimu wa shariya za dini wakwamba kuwa kwanza ajuzi aludi Aliyasi?"

¹² Insa akijibu: "Ndi kweli kuwa Aliyasi akijuzi anze kuja, antengezere vinu piya Binadamu wa Binguni. Fala vyândikiwa novyo kuwa Binadamu akuja kutabika na kukejeliwa, sivyo?

¹³ Kusema kweli, omi nukwambirani kuwa Aliyasi[‡] kâja futi na wantenda piya vyawasakire vyonse kamba vyavyândikiwe kuhusu iye."

Insa amponesa nnemba wakumilikiwa na jini

¹⁴ Paafikire karibu ya wanafunzi ware, wakija wanu wengi wakiwazunguriza, na wanlimu wa shariya wengine wakikaidiyana nawo.

¹⁵ Mpunde noure, wanu ware, pawammonire Insa, wakitajabu pakulu, wakituwa wakuka wakinkomaza.

¹⁶ Insa akiwadairi: "Umwe mwankukaidiyana nawo kinani?"

¹⁷ Ákiwepo mwananlume mmoja kati ya wanu ware akijibu: "Mwanlimu, nija nawo mwanangu-yu, iye kâpatiwa na jini bubu.

¹⁸ Daima jini paampata ponse arefyia pansi. Nnemba-yu akwanza kulawa makovu kukanywa, kutafuna meno, na aawa na nguvu. Niwalebelwa wanafunzi wako-wa wantu-wise jini-yu, awakidirire."

¹⁹ Insa akiwajibu javi: "Ha! Kizazi sacamini! Nukwikala namwe mpaka rini? Nukuhitamilini mpaka rini? Njoni naye nnemba-yo kuno."

²⁰ Ewo wakuka naye. Jini ire nakummona Insa, mpunde noure kangwisira pansi nnemba ire. Iye akinyongoloka kuno akilawa makovu nkanywa.

²¹ Insa akindairi wawaye ire: "Nowu ulwere-wu umwanza rini?"

Iye akijibu: "Umwanza tangu ári kisimana.

²² Mara nydingi zawenye, jini angwisira pamoto na mmaji, kalangela amulaye. Basi, twontere utungu! Ukkidiri, tisaidiye!"

²³ Insa akinjibu, akamba javi: "Sababuni kwamba 'ukikidiri'? Piya vikidirika ka mwenyé kwamini."

²⁴ Kwa mpunde noure, wawaye ire akijibu: "Omi nukwamini, fala nisaidiye nisiwe na dana tena!"

²⁵ Insa paawanang'anize wanu ware, kawawona kuzidi kwengezekwa. Basi akinsutumu jini ire, akamba: "Jini untenza bubu na kewewe nnemba-yu, omi nukwamuru unlawe sambi noppa. Usishubutu kumwingira tena!"

²⁶ Jini ire akikuwa, akinsasanya kanguvu, akinlawa, akimwasa kamba mufwi. Anta na wengi wakidaniza kafwa.

²⁷ Fala Insa akinkola nkono, akinlamusa, neye akimira.

²⁸ Airini, Insa pengire nnyumba, wanafunzi wake wakindairi cembe: "Ofwe atikidirire kuntuwisa jini ámpatire ire, sababuni?"

²⁹ Insa akiwajibu: "Ire jini ire atuwisiwa kwa duwa tu basi[§]."

Insa asowera tena kuhusu kufwa na kufufuka kwake

* 9:1 Ona Matwaya 17:1-11. † 9:11 Ona Malakiya 4:5. ‡ 9:13 Aliyasi epa mana ake ndi Yahaya mwenyé Koza.

§ 9:29 Waraka nyengine zisema: "pamoja na kufunga".

³⁰ Insa na wanafunzi wake, nakulawa pare, wakipita kati-kati ya Galileya. Iye avikimwajibu kuwa munu ejewe mahala pare,

³¹ kamana akiwafunda wanafunzi ware, akiwambira javi: "Binadamu wa Binguni agabiziwa mmakono mwa wanadamu, newo wamulaya. Fala bandi ya kuulaiwa, muda wa suku natu, iye afufuka."

³² Ewo awakereriwa caakamba, na wakopa kundai.

Mwaha kuhusu munu bora kati ya wanafunzi

³³ Wakifika Kafarnaumu. Pawafikire ukaya, Insa akiwadairi wanafunzi ware: "Munjira mure umwe mukikaidiyana kinani?"

³⁴ Fala ewo wakinyamala, konta wakikaidiyana munjira kuwa nani ári bora.

³⁵ Noparepare, Insa akikala, akiweta wanafunzi kumi na wawiri ware, akiwambira: "Ikiwa munu-yo asaka awe ntanzi, ajuzi ariture kuwa wa mwinsho, awatumike wenzive piya."

³⁶ Ikisa, Insa akinkola kisimana mmoja akimwimisa kati yawo, akimpinga mmakono, akiwambira:

³⁷ "Munu asaka kuwa onse ampokérera kisimana kamba-yu, kwa zina rangu, kanipok-erera omi. Na anipokérera omi, kusema kweli aanipokerera omi fala ampokerera Baba wangu ári mbinguni anipereke omi."

Munu satilumbata ofwe kawa upande wetu

³⁸ Yahaya kamwambira Insa: "Mwanlimu, timmona mwananlume mmoja akiwatuwisa mashetwani kwa zina rako. Tinkataza konta aari munkonjo mwetu."

³⁹ Insa akimwambira javi: "Musinkataze! Aapo munu aténda maajuza kwa zina rangu ikisa kanisowerera vibaya.

⁴⁰ Kamana munu satilumbata ofwe, kawa upande wetu.

⁴¹ Munu akupani kopo ya maji kwa kuwa kawa upande wa Almasihi, nukwambirani kweli aakosa futi kupata thawabu yake."

Usiwakorese wenziwo dambi

⁴² Akizidi kwamba: "Munu mmojawapo ankósesa ewa wasimana mmojawapo wanámini-wa, ndi fadari afungiriwe riwe rakupalaza nsingo, atosiwe kati-kati ya bahari.

⁴³ Novyo, ikiwa ukukósesa ndi nkono wako, tupula nowo. Fadari ubadilike wingire mainsha a milele, koliko kuwa na makono mawiri kuka Jahanamu kauri moto sauzimika tena.

⁴⁴*

⁴⁵ Ikiwa ukukósesa ndi mulu wako, tupula nowo. Fadari uwe kitewe wingire mainsha a milele koliko kuwa na maulu mawiri kwefiwa Jahanamu.

⁴⁶†

⁴⁷ Ikiwa riso rako rimojawapo ndi rukukósesa, kotopola noro. Fadari kwingira muufalume wa Mwenyezimungu na riso rimoja basi, koliko kuwa na maso mawiri kwefiwa Jahanamu.

⁴⁸ Eko nvunyo awafwa wala moto-wo auzimika.

⁴⁹ Kamana kila munu ataiwa munyu kwa moto.‡

⁵⁰ Munyu ufái, ulunga cakurya, fala ikiwa munyu ulamwa cilungiriwa kinani? Basi mujuzi muwe kamba munyu§. Piya inshini kwa salama munu na mwensiwe."

10

Kulombana na kwasana

¹ Ikisa Insa akilawa mahala pare, akukirira makaya ya Yudeya na ng'ambu ya muto wa Yordani. Akijumana nawo novyo tena wanu wengi, na kamba vyazowerere, akikola wakufunda.

² Mafarizeu wakinfika karibu wakindairi javi: "Iwapo haki nlume kumwasa nkawake?" Wandairi javyo konta wakisakula wankorese.

³ Insa akijibu, akamba: "Musa kakwamuruni mwaja?"

⁴ Ewo wakijibu: "Musa karuhusu nlume antaliki nkawake, ushahidi wa kumwasa."

* ^{9:44} Aya-yi aipo mmandiko mengi meema. [Eko nvunyo awafwa wala moto-wo auzimika.] † ^{9:46} Aya-yi aipo mmandiko mengi meema. [Eko nvunyo awafwa wala moto-wo auzimika.] ‡ ^{9:49} Wanu wengi wadaniza kuwa mana ake javi: Wanu sawari wafulati wa Insa wahukumiwa na moto Jahanamu. Wafulati wa Insa watabika ipate waswafiwe.

§ ^{9:50} Munyu ndi alama ya miyadi ya kupatana na Mwenyezimungu. Ofwe, kwa sababu ya miyadi-yo, ikiwa tawanu wa Mwenyezimungu, tijuzi titenda kamba wanu wake. Ona Kulawa 30:35.

⁵ Insa akiwambira: "Musa kândika eyi ámuri-yi kwa sababu ya myoyo yenu kuwa migumu.

⁶ Fala tangu mwanzo wa kumba, Mwenyezimungu kamumba nlume na muka.

⁷ Ndimana, mwananlume awasa wawaye na mamaye, alungana afulatana pamoja na nkawake,

⁸ wo-wowiri wakuwa mwiri mmoja*, awawa futi wawiri tena, ila mwiri mmoja tu basi.

⁹ Kwa javyo, kinu caaluganise Mwenyezimungu, munu asasanise."

¹⁰ Airini, Insa paákiwa ukaya na wanafunzi wake, ewo waludira kundairi kuhusu noure mwahe ure.

¹¹ Iye kawambira: "Mwenye kumwasa nkawake akinlomba mwengine, kawakuzinga naye.

¹² Na ikiwa mwanamuka kamwasa nlumake, akilombiwa na nlume mwengine, neye novyo kawankuzinga."

Insa awajanliya wasimana

¹³ Sambi wanu wengine waja nawo wana awakumbure, fala wanafunzi ware wakiwasutumu wanu ware.

¹⁴ Iye paawawonire, akikimiwa na wanafunzi wake pakulu futi, akiwambira javi: "Waseni wasimana-wo waje kwangu omi kuno! Musiwakataze! Kamana ufalume wa Mwenyezimungu wanu kamba ewa ndi wawo.

¹⁵ Nukwambirani kweli kuwa munu saapokerera ufalume wa Mwenyezimungu kamba kisimana, visaka kuwa vyonse emo engira."

¹⁶ Ikisa wasimana ware akiwakola makono, akiwajaniya kuno akiwatula makono.

Matajiri na ufalume wa Mwenyezimungu

¹⁷ Insa, nakulongoza njira, mwananlume mmoja akintuwirira, akikokora mbere yake, akindairi: "Mwanlimu mwema, kupata mainsha a milele, nijuzi kutenda kinani?"

¹⁸ Insa akinjibu: "Sababuni kunita mwema? Hapano mwema ila Mwenyezimungu tu basi.

¹⁹ Ukwijiwa ámuri zamba javi: usimulaye munu, usizinge, usiwe, usiseme ushahidi wa ulongo, usitende udanganyifu, na umwinshimu wawayo na mamayo."

²⁰ Iye akinjibu: "Mwanlimu, ezo ámuri-zo ndi zanifulata tangu unemba wangu."

²¹ Insa akinang'aniza ka kumpenda pakulu, akimwambira javi: "Ciwapo kinu cukubakire. Uka, ukauzanye vyaúri navyo piya, uwape masikini. Kwa javyo, ukuwa nawo mali mbinguni. Njo, unifulate."

²² Nakusikira usowezi ure, akilawa auzunike pakulu futi, konta ákiwa tajiri pakulu.

²³ Insa akinang'aniza nanyenje ire, akiwambira wanafunzi wake ware javi: "Virigariga pakulu matajiri kwingira muufalume wa Mwenyezimungu!"

²⁴ Wanafunzi, pawasikire usowezi ure, wakashanga. Fala Insa akisowera tena: "Wanango, virigariga pakulu kwingira muufalume wa Mwenyezimungu!"

²⁵ Raisi pakulu ngamiya kupita kupenya pakipenyo ca singano koliko tajiri kwingira muufalume wa Mwenyezimungu."

²⁶ Wanafunzi ware watajabu pakulu, wakidairiyana watupu: "Kwa javyo, nani aja kuvushisha?"

²⁷ Insa akiwanang'aniza rungu-rungu, akiwambira: "Virigariga ka wanadamu. Fala ka Mwenyezimungu avirigariga, konta kwake iye, piya vikidirika."

²⁸ Peduru akanza kumwambira Insa javi: "Ona, ofwe tasa piya vinu, tiwankukufulata."

²⁹ Insa akijibu: "Nukwambirani kweli kuwa kila mwenyé kwasa nyumba, wanduze, walumbuze, mamaye, wawaye, wanawe, au inti yake, kwa sababu yangu omi na kwa sababu ya Habari Ngema,

³⁰ apata mara miya sambi-pa nowu wakati-wu, manyumba, wanduze, walumbuze, mamaze, wanawe, na inti, pamoja na kulumbatiwa. Na ulumwengu uja-wo, apata mainsha a milele.

³¹ Na wengi wari watanzi sambi-pa wakuja kuwa wamwinsho, na wamwinsho wakuja kuwa watanzi."

Insa asowera tena kuhusu kufwa na kufufuka kwake

³² Sambi ewo wari munjira wakuka Yerusalem, Insa kalongorera. Wakinfulata piya washanga na wanu wengine walongozane nawo wakiwa na wofii. Basi, Insa akiweta mara nyengine tena wanafunzi kumi na wawiri ware akanza kuwambira piya vyuka kunkuna Yerusalem.

³³ Akiwambira javi: "Sikirizani! Tankuka Yerusalem, Binadamu wa Binguni agabiziwa walongozi wakulu wa dini na wanlimu wa shariya. Ewo wakuka kunlamula aulaiwe na wampereka ka Sawari-Mayahudi.

³⁴ Ewo wakuka kunshupa, kunsunira mata, kumwibya, na kumulaya. Fala muda wa suku natu, iye afufuka."

Insa afunda kuhusu kuudumiyanu munu na mwensiwe

³⁵ Ikisa, Yakobu pamoja na Yahaya, wana wawiri wa Zebedeyu, wakimukira Insa, wakimwambira: "Mwanlimu, tisaka catukulebela conse, utitendere noco."

³⁶ Insa akijibu: "Musaka nukutendereni kinani?"

³⁷ Ewo wakimwambira: "Pausaka kuwa muufalume wako wa utukufu, ofwe-pa mmoja akwikare upande wa nkono sonto na mwengine upande wa nkono nriro wako[†]."

³⁸ Insa akijibu: "Umwe anta camulebela amwijiwa. Mukidiri kunywa kikombe ca ninywa omi au mukidiri koziwa kamba vyanoziwe omi[‡]?"

³⁹ Ewo wakinjibu: "Aye, tikidiri!" Basi, Insa akiwambira: "Mukuja kunywa kikombe caninywa omi, na koziwa kanoziwe omi nomwe mukuja koziwa."

⁴⁰ Fala kwikalwa upande wa nkono-nriro au nkono-sonto wangu sumi namuru kwikaza ila wakwikaziwa watengezeriwe kwikalwa."

⁴¹ Wanafunzi wengine kumi ware pawejiwe cawakilebela, wakiwakimwira Yakobu na Yahaya.

⁴² Basi, Insa akiweta wanafunzi ware, akiwambira: "Umwe mukwijiwa kuwa inti piya mafalume ndi wawatawala wanu kwanguvu, na wakulungwa wawo ndi walavya ámuri zakuwatuma.

⁴³ Falakini kati yenu umwe, sivyaviri javyo. Kusema kweli, asakula awe nkulu, akuwa ntumisi wenu.

⁴⁴ Na kati yenu asaka kuwa awe wakwanza siti awe ntwana wa piya-mwe.

⁴⁵ Konta na Binadamu wa Binguni novyo, aajire kutumikiriwa ila kaja kutumika na kupereka mainsha ake kuwa maripo, awavushe wanu wengi."

Insa amponesa munu sawona

⁴⁶ Basi, ewo wakifika Yeriko. Insa ákiwa na wanafunzi wake pamoja na junudi ya wanu wengi wawenye. Pawalawire Yeriko, nzimola munu sawona wakwitiwa Bartimeu (mana ake mwana wa Timeu), kekala nanyenje ya njira.

⁴⁷ Paasikire kuwa Insa nNazareti ndi ari kupita, iye akanza kukuwa: "Insa mwana wa Daudi, niwonere utungu!"

⁴⁸ Wengi wakimwambira anyamare. Fala iye akizidi kukuwa pakulu-pakulu: "Mwana wa Daudi, niwonere utungu!"

⁴⁹ Insa paansikire, iye akimira, akamba: "Mwiteni aje kuno." Basi, ewo wakimwita kipofu ire, wakimwambira: "Iwa radi! Lamuka, kwankwitiwa."

⁵⁰ Kipofu Bartimeu ire akiwula vazi rake akefya pansi, akilamuka akuka ka Insa.

⁵¹ Insa akindairi: "Uwe usaka nukutende mwaja?" Iye akamba: "He, mwanlimu! Nisaka niludire kuwona!"

⁵² Insa akimwambira: "Uka! Kwamini kwako kukuponesa!" Kwa mpunde noure, akiludira kuwona tena, neye akikola kunfulata noire njira ire.

11

Insa akwingira kaya ulu ya Yerusalem

¹ Insa pamoja na wanafunzi wake wari karibu ya Yerusalem, pepi ya Betifage na Betaniya pamwango wa Mizaituni, iye akiwatumua wanafunzi wawiri,

² akiwambira javi: "Ukani mpaka kaya iri mbere ire. Mukifika, munsingana buru afungiriwe pamuti, tangu saanapandiwa na munu. Munfungure, muje nawo kuno.

³ Ikiyu munu kakudairini camutenda-ci kinani, mwambireni kuwa Mwenye ndi ari kunsakula, anludisa sambi-pa."

⁴ Ewo wakuka, wakinsingana buru afungiriwe pamuti panja karibu ya nryango, wakin-fungula.

⁵ Wanu wengine wemire nopare wakiwadairi: "Mбана mwankunfungula buru-yo?"

⁶ Ewo wakiwajibu kamba vyawatumiwe na Insa, wakiwasa wakuka vyawo.

⁷ Ikisa, wanafunzi ware wakintwala buru ire wakuka naye ka Insa, wakitandika makapa awo julu ya buru ire, na iye akimpanda.

[†] **10:37** Wakidanizira kuwa mikono miwiri ya Almasihi mbinguni ndi mahala pawekala wanu bora, wakupokerera cewo bora. [‡] **10:38** "Kunywa kikombe" mana ake kukubali kutabikira kinu caufulata na mana a "koziwa" ndi kukubali kufwira kinu caufulata.

⁸ Wanu wengi wawenye wakitandika mavazi awo munjira mure, na wengine waki-tandika makuti a mitende awakisinja a mmamasamba.

⁹ Walongorere mbere na wakiwafulata wakimba pakulu-pakulu:

“Hozana! * Ajanliiwe ári kuja kwa zina ra Mola!

¹⁰ Ujanliiwe ufalume usaka kuja-wo,
ufalume wa babu yetu Daudi!

Hozana mbingu ya mwinsho!”

